







Anansi na hekima


-  Ghanaian folktale
-  Wiehan de Jager
-  Mutugi Kamundi
-  Kiswahili
-  Level 3

(imageless edition)






Hapo zamani za kale, watu hawakujua chochote. Hawakujua kupanda mimea, hawakujua kushona nguo, wala hawakujua kuunda zana za chuma. Nyame, mungu aliyekuwa mbinguni, ndiye aliyekuwa mwenye hekima zote za dunia. Alihifadhi hekima hiyo kwenye chungu cha udongo.




Siku moja, Nyame aliamua kumpa
Anansi chungu hicho cha hekima. Kila
Anansi alipotazama ndani ya chungu
cha udongo, alijifunza jambo jipya.
Alifurahi sana!




Anansi mlafi alinong'ona moyoni,
“Nitakificha chungu hiki juu ya mti
mrefu ili nikifaidi mwenyewe.”


Akasokota uzi mrefu na kuuzungusha
kwenye chungu. Kisha, akajifunga
tumboni. Akaanza kupanda kwenye
mti. Lakini ilikuwa vigumu kupanda
kwenye mti huku chungu kikimgonga
magotini kila mara.



Wakati huo wote, mwanawe alikuwa amesimama chini ya ule mti akimtazama baba yake. Akamwambia, “Baba, si ingekuwa rahisi kupanda endapo ungekifungia chungu mgongoni?” Basi Anansi akajaribu kukifungia chungu kilichojaa hekima mgongoni mwake, na kweli ikawa rahisi zaidi.



Punde tu alifika juu ya mti, aliwaza,
“Natakiwa kuwa ndiye mwenye hekima
zote, lakini hapa mwanangu ndiye
mwenye akili kuliko mimi.” Anansi
alikasirishwa sana kiasi kwamba
alikitupa kile chungu chini ya mti.



Chungu kilivunjika vipandevipande pale chini. Hekima zikawa za bure kwa mtu yeyote kujichukulia. Na hivyo ndivyo watu walivyojifunza kulima, kushona nguo, kuunda zana za chuma, na mambo yote mengine ambayo watu wanajua kuyafanya.



Storybooks Canada

storybookscanada.ca

Anansi na hekima

Written by: Ghanaian folktale

Illustrated by: Wiehan de Jager

Translated by: Mutugi Kamundi

This story originates from the African Storybook (africanstorybook.org) and is brought to you by Storybooks Canada in an effort to provide children's stories in Canada's many languages.



This work is licensed under a Creative Commons
[Attribution 3.0 International License](http://creativecommons.org/licenses/by/3.0/).